OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKODNARI LUHOTA,
S.L.P. 2455,
IRINGA.

NDG_____
S.L.P. _____
_____

YAH : KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUHOTA 2021

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari LUHOTA. Hongera sana na karibu Luhota Sekondari.

MAHALI ILIPO SHULE
Shule ya sekondari Luhota ipo katika kijiji cha Kilambo yapata umbali wa km 3.1 toka Kilambo stendi eneo la sokoni. Shule hii ni ya mchanganyiko na ya kutwa kwa wasichana na wavulana.

KUANZA MUHULA WA MASOMO
Shule itafunguliwa rasmi tarehe ……..unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ……hadi tarehe …….kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana kwa zoezi nzima la usajiri. Ikumbukwe kuwa ukichelewa nafasi yako itatolewa kwa mtu mwingine mwenye sifa kama yako ambaye hajapata nafasi awamu hii, zingatia hilo na ufanye maandalizi kuanzia sasa.

KUSAJIRIWA
Wakati wa usajiri unatakiwa kuwa na mambo yafuatayo:-

A. MAELEKEZO MUHIMU JUU YA WJAIBU WA MZAZI NA MWANAFUNZI (WARAKA WA ELIMU NA.6 WA MWAKA 2015)

3.6 **WAJIBU WA MZAZI**

(i) Kununua sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo madaftari na kalamu na chakula kwa wanafunzi wa kutwa.
(ii) Kugharamia matibabu kwa watoto wao.
(iii) Kulipia nauli ya kwenda shule na kurudi kwa wanafuzi wa kutwa na mwanafunzi wa bweni wakati wa kufunga na kufungua shule.
(iv) Kununua magodoro, shuka, vifaa vya usafi kwa wanafunzi wanaosoma shule za bweni na wanaoishi katika Hostel zinazotumiwa na serikali na
(v) Kukemea na kutoa taarifa kuhusu mienendo inayokwenda kinyume na elimu msingi bila mlipo.

B. WANAFUNZI;
Wanafunzi ambao ndio walengwa wa Elimu msingi bila malipo wanamajukumu yafuatayo:-
(i) Kwenda shule na kuhudhuria masomo kulingana na ratiba ya shule.
(ii) Kuwa na maadili mema wakati wote na hivyo kuacha kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa kanuni mbalimbali za shule na sheria za nchi.
(iii) Kutoa mrejesho kwa mzazi/mlezi wa kike walichojifunza ili wafahamu na kuwasiaidia watoto wao katika maendeleo ya elimumsingi kadri watakavyoona inafaa na

(iv) Kutoa mrejesho kwa wazazi/walezi kuhusu jambo lolote linaloagizwa kinyume na maagizo ya elimu msingi bila malipo.

SARE ZA SHULE

Wasichana

- Blauzi nyeupe mikono mifupi 2 (kitambaa cha tetroni chenye mng'ao mzuri)
- Sketi 2 kitambaa kizito rangi ya bluu bahari mshono wa rinda boksi
- Soksi nyeupe pea 2
- Sweta mbili (2) rangi ya damu ya mzee yenye shingo ya "V" yasiyo na vifungo
- Viatu vyeusi vya ngozi na si raba viwe na kisigino kifupi na vya kufunga kwa kamba. Vinginevyo vitanyang'anywa na kuchomwa moto

NB : Kuvaa sketi ambayo haivuki magoti itakuwa ni kosa kubwa la kusimamishwa masomo na hatua kali za kisheria zitachukuliwa. Mzazi kagua mara kwa mara urefu w sketi ya mwanao.

Wavulana

- Shati nyeupe mikono mifupi 2 (kitambaa cha tetroni chenye mng'ao mzuri)
- Suruali 2 kitambaa rangi ya bluu bahari iwe na marinda mawili
- Soksi nyeupe pea 2
- Sweta pea mbili rangi ya damu ya mzee yenye shingo ya "V" yasiyo na vifungo
- Viatu vyeusi vya ngozi na si raba viwe na kisigino kifupi na vya kufunga kwa kamba. Vinginevyo vitanyang'anywa na kuchomwa moto. Ni kataza kabisa kuvaa viatu vilivyo chongoka mbele (four angle) au vyenye chuma mbele (buti)

NB : Mzazi simamia ushonaji wa suruali ya mwanao fundi apime saizi ya kiuno na ashobne suruali ya kuvalia kiunoni na si makalioni au tumboni, Suruali nyembamba na zilizochongoka chini itakuwa ni hasara yako na haitakubalika kwa namna yeyote ile.

NGUO ZA MICHEZO

Ikumbukwe kuwa kila siku ya Ijumaa jioni itakuwa ni siku ya michezo. Mwanao atatakiwa kushiriki kikamilifu katika michezo akiwa na mavazi rasmi kama vile:-

Wasichana

1. Track suit rangi nyeusi yenye michorizi myeupe (isiyobana)
2. Raba za michezo

Wavulana

1. Bukta na furana rangi ya bluu isiyo na maandishi yoyote
2. Viatu vya kuchezea mpira visivyo na chuma au soli yenye meno ya plastiki

NB : Kila mwanafunzi atalazimika kushiriki moja au zaidi ya michezo iliyopo shuleni na ikumbukwe kuwa kutoshiriki katika michezo litakuwa ni kosa.

MASOMO YAFUNDISHWAYO

Ufikapo Luhota sekondari utajifunza masomo yafuatayo

CIVICS, KISWAHILI, ENGLISH, HISTORY, BIOLOGY, GEOGRAPHY, PHYSICS, CHEMISTRY, BASIC MATHEMATICS NA VIOPINDI VYA DINI

Unatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo:-

1. Daftari kubwa 10 za masomo ya darasani (counter book 2Q pekee)
2. Kalamu za kutosha
3. Mkebe na rula
4. Dictionary kila mtoto aje nayo ikiwa imeandikwa jina lake na itakaguliwa

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

1. Kufika shuleni siku zote na kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa kwa kadri ya ratiba ya siku husika
2. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule pasipo shuruti.
3. Kuzingatia ratiba ya shule kila wakati.
4. Kuvaa sare ya shule wakati wowote unapotakiwa
5. Kuwa na heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla
6. Kusimama wakati wa kusalimia, kuwapokea wanaokuzidi umri wanapopita ulipo
7. Kutumia lugha nzuri muda wote na kwa mtu yeyote lugha za matusi, vitisho havitavumilika
8. Kumsaidia mwanafunzi mwenzio na kushirikiana naye katika shughuli mbalimbali za kimasomo.
9. Kumkaribisha mgeni na kumuelekeza sehemu husika kadri ya shida yake au kufikisha kwa mwalimu wa zamu,
10. Ni marufuku kuwasiliana na mgeni yeyote bila kibali cha mwalimu
11. Simu, camera, na redio havitakiwi maeneo ya shule. Amri vinginevyo vitanyang'angwa na kuteketezwa bila huruma.
12. Ni marufuku kutoa taarifa yoyote inayohusu shule kwenye chombo cha habari au mwandishi wa habari kwa namna yoyote ile. Ikigundilika litakuwa ni kosa kubwa.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi, na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga au kupigana
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
11. Kutoa mimba au kushiriki kutoa mimba
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kugoma, kuchochea, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
14. Kuwa na simu ya mkononi au laini ya mtandao wowote

CHAKULA CHA MCHANA

Chakula cha mchana kitaandaliwa shuleni kwa wanafunzi wote wa kutwa na ni lazima kwa mujibu wa maelekezo ya serikali hivyo mwanao anapokuja shuleni hakikisha anakuja na

(I) Mahindi debe 3 kwa mwaka mzima

(II) Mharagwe kg 20 (platic moja) kwa mwaka mzima

(III) Pesa taslimu 15,000/= kwa ajili ya mpishi, gharama za mashinenI na viungo kwa mwaka mzika

HUDUMA YA HOSTELI:

Kwa yule anayehitaji mwanae akae chini ya uangalizi maalumu, kuna huduma ya Hostel kwa wasichana tu. Kwa kuwa nafasi ni chache kwa anayehitaji afike shuleni apate fomu maalumu ya kujiunga Hostel au piga simu 0719 565066 au 0763 288433

Nakutakia maandalizi mema

MWL. A. KISONGA (0759 050790)
Mkuu wa shule